Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Kuwasha Taa Makaburini

Kuwasha taa kwenye makaburi ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu, jambo ambalo mawahabi wanadai kuwa ni haramu, halina umuhimu mkubwa kwa kuwa dalili pekee waitumiayo ni ile hadithi aliyoitaja An-Nasai kutoka kwa Ibn Abbas kwamba, "Mtume [s] amewalaani wanawake wanaozuru makaburi na wanaoyafanya kuwa ni misikiti na wale wanaayawasha taa."1

Hadithi hii na nyinginezo mfano wa hii zinahusika tu kama kuwasha taa huko kutakuwa ni kupoteza na kufuja mali au kutasababisha kujifananisha kwa baadhi ya nyumati na mataifa na dini batili, kama alivyolionyesha jambo hilo Al-Allamah as-Sindi katika sherehe ya hadithi hii aliposema:
"Na katazo hilo ni kwa kuwa (kuwasha taa) husababisha kupoteza mali bila manufaa."2

Ama kama lengo litakuwa ni kuwasha taa kwa ajili ya kusoma Qur'an, kuomba, kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu, kuswali na mengineyo katika mambo mustahabbu na wajibu pamoja na manufaa yanayo kubalika kisheria, basi haya yote hayana matatizo kabisa,

"***Saidianeni katika mema na uchamungu.***" Qur'an, 5:2.

Basi vipi itakuwa haramu? Ilivyo ndivyo ni kwamba, kuwasha taa makaburini ni jambo mustahabbu kisheria na linapendeza kiakili.

1. Sunan An-Nasai, juz. 3, uk. 77.
2. As-Sunan An-Nasai. juz. 3, uk. 77, chapa ya Misri. Na juz. 4, uk. 95, chapa ya Beirut, Sharh Jamiu Saghir, juz. 2, uk. 198

Source URL:
https://www.al-islam.org/uchunguzi-juu-ya-uwahhabi-ayatullah-jafar-subhani/kuwasha-taa-makaburini#comment-0